



Fair Work Commission

Sisi ni mahakama huru ya mahusiano ya mahali pa kazi ya Australia. Tunasaidia wafanyakazi na waajiri kutatua matatizo kazini. Hii inajumuisha:



Kufukuzwa kazi
bila haki



Uonevu



Unyanyasaji wa
kingono



Ubaguzi



Migogoro ya
haki za mahali
pa kazi

Pia:

tunaamua kima cha chini cha mshahara kitaifa

tunaweka masharti ya chini zaidi ya ajira kwa baadhi ya wafanyakazi

tunaidhinisha mikataba ya biashara

tunadhibiti mashirika yaliyosajiliwa, kama vile vyama vya
wafanyakazi na mashirika ya waajiri

Kazi yetu ni kusaidia mahusiano rahisi, ya haki, na yanayobadilika mahali pa kazi kwa wafanyakazi na waajiri.

Kwa habari kuhusu malipo, likizo na stahili zingine tembelea tovuti ya Fair Work Ombudsman kwa www.fairwork.gov.au



Kutatua masuala ya mahali pa kazi

Unapotuuliza tusuluhishe suala la mahali pa kazi, unaanza mchakato wa kisheria.

Utahitaji kujaza fomu inayoelezea suala au tatizo hilo. Nenda kwa 'Apply or Lodge' kwenye tovuti yetu. Tutashiriki fomu yako na mtu mwingine anayehusika. Fomu yake pia itashirikiwa nawe.

Tutajaribu kukusaidia kukubaliana juu ya suluhisho.

Ikiwa hii haitafanya kazi, unaweza kutuuliza tukuamulie matokeo kwa niaba yako. Hii ni kama kuwa kwenye kesi mahakamani. Uamuzi wetu ni wa kisheria.

Msaada katika lugha yako

Unaweza kutumia Translating and Interpreting Service (TIS) kuweza kutupigia simu.



Piga simu

131 450

Ni huduma ya bure.

Mwambie mtu wa mapokezi:

- lugha yako – ili akuunganishe na mkalimani
- jina letu – Fair Work Commission (Tume ya Usawa wa Kazi)
- namba yetu ya simu – 1300 799 675

Tunaweza pia kupanga mkalimani ikiwa unahitaji kushiriki katika mkutano au usikilizaji.

Ushauri wa bure wa kisheria

Iwapo unahitaji usaidizi wa kuamua la kufanya, tuna huduma ya kisheria bila malipo kwa wafanyakazi na biashara ndogo ndogo. Tazama kwenye 'Workplace Advice Service' kwenye tovuti yetu.

Huduma hii inaweza kusaidia kwa kufukuzwa kazi kwa njia isiyo ya haki, ubaguzi, uonevu na unyanyasaji wa kingono kazini.